

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**  
ISO 9001:2015 CERTIFIED



## TAARIFA KWA UMMA

### MAOMBI YA UHAMISHO WA HISA

Taarifa inatolewa kwa Umma kwamba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imepokea ombi la uhamisho wa hisa kutoka kwa kampuni ya Habari Node Limited ambapo inahusisha uhamisho wa hisa zote za mwombaji kwenda kwa kampuni ya Mawingu Networks Limited na Bw. Farouk Ramji. Taarifa za hisa zinazokusudiwa kuchukuliwa ni kama ifuatavyo: -

NA.	JINA LA ANAYEHAMISHA HISA	JINA LA ANAYEHAMISHIWA HISA	AINA YA LESENI	WANAHISA / URAIA	HISA %
1.	Habari Node Limited	Mawingu Networks Limited	Leseni ya Kimkoa ya Miundombinu ya Mawasiliano	Mawingu Networks Limited (Mumauritius)	99.998
		Mr. Farouk Ramji	Leseni ya Kimkoa ya Huduma ya Mifumo Tumizi	Bw. Farouk Ramji (Mkanada)	0.002

Kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta, Sura 306 ya sheria za Tanzania, maoni ya kimaandishi yanakaribishwa kutoka kwa yeyote kuhusiana na utoaji wa leseni kwa muombaji na yafike TCRA ndani ya siku kumi na nne (14) tangu siku ya kutoka tangazo hili. Maoni yaliyopokelewa yatazingatiwa na TCRA itakapokuwa inayafanyia kazi ombi hili.

**Maoni yatumwe kwa:**

Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,  
S.L.P 474,  
Postikodi 14414 DAR ES SALAAM.  
Simu: +255 22 241 2011-2  
Faxsi: +255 22 2412009  
Barua pepe: [dq@tcra.go.tz](mailto:dq@tcra.go.tz)

Imetolewa Tarehe **29 Julai 2024.**

Dkt. Jabiri K. Bakari  
**MKURUGENZI MKUU**